# Samaki wanaoelea wazua taharuki ufukweni

NA IRENE MWASOMOLA

TAHARUKI iliibuka jana kwenye fukwe za bahari ya Hindi eneo la Aga khan viwanja vya Gymkhana Jijini Dar es Salaam baada ya kuonekana samaki wanaotoka wenyewe ndani ya bahari huku wakiwa wazima.

Gazeti hili lilifika kwenye fukwe hizo na kushuhudia badhi ya wananchi wakiokota samaki waliokuwa wanazagaa pembezoni mwa maji katika eneo hilo.

Wakizungumza na gazeti hili jana baadhi ya mashuhuda na watu waliokuwa wanaokota samaki hao walisema ni mara ya kwanza kwenye eneo hilo kuonekana samaki wakiwa wanaelea wenyewe baharini.

Shanibi Swalehe, Mfanyabiashara wa madafu pembezoni mwa fukwe hizo alisema kuliibuka upepo wenye mawimbi makali na kusababisha maji kujaa tangia majira ya saa nne asubuhi.

Naye Shabani Hoseni mkazi wa Kigamboni ,alisema aliokota samaki zaidi ya kilo tano lakini badhi ya jeshi la polisi walifika eneo hilo na kuwazuia wananchi wasiendelee kuokota samaki hao kwaajili ya usalama wao.

Aidha, Meneja wa soko la samaki feri Denis Mrema,alisema taarifa hizo ni za kweli kwa kushirikiana na jeshi la polisi walifika eneo la tukio na kuchukua sampuli na kupeleka kwa mkemia mkuu ili kujua kama hao samaki ni salama kwa matumizi ya binadamu.

"Habari ni ya kweli na tumeteketeza badhi ya samaki, na sampuli zimechukuliwa ili kupelekwa kwa mkemia mkuu" alisema.

Aidha Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salam Jumanne Muliro alipoulizwa juu ya taarifa hizo alisema hausiki nazo.

"Mimi na samaki wapi na wapi jeshi la Polisi na samaki wapi na wapi waulize watu wa uvuvi,mimi niulize masuala ya waharifu na majambazi"alisema.

Uhuru Uk.3, Julai 22,3021

Scanned with CamScanner

a la uzalishaji mifugo la Taifa Mabuki lilianzishwa

# Kuzeeka kwa ng'ombe wazazi kwapunguza uzalishaji mifugo

**NA PETER KATULANDA,** Misungwi

SHAMBA la Uzalishaji Mifugo la Taifa Mabuki, lililopo wilayani hapa, mkoani Mwanza, limepunguza uwezo wa uzalishaji kutokana na kuzeeka kwa ng'ombe wazazi.

Imeelezwa ng'ombe aina ya nyati maji walioko katika shamba hilo, wanaendelea kupoteza maumbile yao ya asili, hivyo nao kukosa mvuto kwa wananchi ambao wangewanunua na kuwatumia kama wanyama kazi.

Kauli hiyo ilitolewa mwisho wa wiki na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti (TALIRI) Mabuki, Dk. Heriel Masawe, alipotoa maelezo kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki.

Alisema ili kuziba pengo la ng'ombe hao, ambao kwa sasa hawana uwezo mzuri wa kuzaa kila mwaka, wanaiomba serikali iwaongeze.

"Waziri, uone uwezekano wa kuongeza ng'ombe wazazi ili kuongeza kiasi cha uzalishaji, idadi ya mitamba inayosambazwa kwa wananchi wafugaji iongezeke na serikali itimize malengo yake ya kuwahudumia wananchi wajikwamue kutoka katika umasikini," alisema.

Dk. Masawe alisema katika kujikwamua kutoka katika umaskini, wafugaji watachangia upatikanaji wa malighafi inayohitajika kwa ajili ya viwanda vya maziwa nchini.

"Kutokana na kuzaliana kizazi kimoja kwa muda mrefu (inbreeding) nyati maji 55 tulionao, wameendelea kupoteza maumbile yao ya asili na kupoteza mvuto kwa wananchi ambao wangewanunua na kuwatumia kama wanyama kazi," alisema.

Aliiomba serikali ione umuhimu wa kununua nyati wengine kutoka nchini Misri au India, ili kuondoa tatizo hilo na ikiwezekana kununua mbegu za nyati kutoka nchi husika ili wazalishe kwa njia ya uhamilishaji.

Kwa mujibu wa Dk. Massawe, idadi ya ng'ombe majike kwa miaka tisa iliyopita imekuwa ikipanda na kupungua na jumla yake katika mabano mwaka 2010/2011 chotara walikuwa 95, borani 803 (898), mwaka 2011/2012 chaotara 85, borani 836 ( 921) na 2012/2013 chotara walikuwa 85, borani 837 (922).

Mwaka 2013/2014 chotara 76, borani 751 (827), 2014/2015 chotara 72, borani 728 ( 800), 2015/2016 chotara 66, borani 654 ( 720), 2016/2017 chotara 46, borani 527 ( 575), 2017/2018 chotara 52, borani 512 ( 564), 2018/2019 chotara 93, borani 523 ( 616) na 2019/2020 chotara 79, borani 701 (780).

Shamba hilo lililoanzishwa mwaka 1967, sasa lina ng'ombe wenye umri tofauti 1,950, mbuzi 302, nyati maji 55 na nguruwe 40 na linakabiliwa na uhaba wa maji safi kwa ajili ya mifugo, uchakavu wa mitambo, magari na nyumba za watumishi ambazo Waziri Ndaki alisema serikali inazifanyia kazi.

Scanned with CamScanner

# Samaki waliokufa wazagaa ufukweni

UKURASA 4

MICHEZO SIMBA

Nipashe Uk.1 , Julai 22,2021

Scanned with CamScanner

# Samaki waliokufa wazagaa ufukweni

**Na Romana Mallya**

SAMAKI waliokufa wameonekana kwenye ufukwe wa Bahari ya Hindi eneo la Aga Khan jijini Dar es Salaam.

Mamlaka za serikali zimekiri kuonekana kwa samaki hao na tayari uchunguzi umeanza kubaini chanzo chake.

Mmoja wa mashuhuda aliyekuwa sehemu ya timu ya maofisa wa serikali waliozuru eneo la tukio jana, aliliambia Nipashe kuwa suala hilo lipo kwenye uchunguzi wa Jeshi la Polisi na mamlaka zingine za serikali na tayari sampuli zimechukuliwa kwenda kwa Mkemia Mkuu wa Serikali.

Ofisa huyo ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini kwa kuwa si msemaji, alisema samaki hao walionekana kwenye eneo hilo Aga Khan.

"Tulijaribu kukusanya na zilifika kilo zaidi ya 150, ila kwa sasa ni mapema kulizungumzia suala hili," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, alipoulizwa kuhusiana na samaki hao, alisema kwa wakati huo hakuwa na taarifa na kuahidi kutuma wataalamu wake kwenda eneo la tukio.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), Dk. Ismail Kimirei, alikiri samaki hao walionekana eneo hilo la ufukwe lakini polisi waliingia kati mwanzoni na waliwapa taarifa maofisa wa Wizara ya Mifugo ambao mara moja walikwenda eneo la tukio.

"Tukafika na watu wa wizara tumechukua sampuli na zingine zimekwenda maabara ya taifa ya wizara na polisi kwa ajili ya kupeleka kwa Mkemia Mkuu, tunasubiri majibu.

"Samaki waliokusanywa walikuwa ni wa aina mbalimbali lakini wengi wao ni watoto na ziliokotwa kilo 160," alisema. Hata hivyo, alisema matukio kama hayo ya samaki kukutwa ufukweni wakiwa wamekufa wakati mwingine hutokea wanapokosa hewa ya Oksijeni baharini.

Alisema mpaka sasa hawajapata taarifa za kuwapo kwa samaki wakiwa wamekufa sehemu nyingine zaidi ya ufukwe uliopo karibu na Hospitali ya Aga Khan.

Scanned with CamScanner

nika kununua mashine za kutotolesha vifaranga vya kuku

# Katambi aagiza manispaa kununua mashine za kutotolesha vifaranga

**NA CHIBURA MAKORONGO, SHINYANGA**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas Katambi, amesema sh. milioni 19 zilizotolewa na wizara hiyo Manispaa ya Shinyanga, zitumike kununua mashine za kutotoleshea vifaranga na kutengeneza chakula cha kuku ili kuwawezesha vijana kuajiajiri.

Katambi ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini (CCM), aliyasema hayo alipotembelea Kata za Chibe na Lubaga zilizopo Manispaa ya Shinyanga, akiwa ameambatana na wakuu wa idara kutoka sekta mbalimbali kujibu changamoto zinazowakabili wananchi.

"Mashine hizo zitakuwa na uwezo wa kutotolesha vifaranga 1,200 kwa siku na kutengenezea chakula cha kuku, vijana watakapojiunga katika vikundi watanufaika, kwani chakula cha kuku watauza, kuku watakapo komaa watauzwa kwa watu nyumbani na hotelini kwani soko lipo la uhakikisa," alieleza.

Alimshauri Kaimu Ofisa Maendeleo na Vijana wa Manispaa hiyo, Charles Luchagula, kuwa fedha hizo wasizikopeshe katika vikundi zinaweza kuonekana hakuna kitu kilichofanyika, bali zitumike kununua mashine za kutotolesha kuku.

Luchagula alikiri kupokea sh. milioni 19 kwa ajili ya mikopo kwa vijana, huku akieleza kwamba mwaka wa fedha wa 2020/2021 zilitengwa zaidi ya sh. milioni 278.3 zilizotumika kukopesha vikundi 22.

Aidha, alisema mwaka huu wa fedha kupitia mapato ya ndani wameweza kutenga zaidi ya sh. milioni 361.2, ambapo wanawake wamepangiwa a zaidi ya sh. milioni 144.5, sawa na kundi la vijana na walemavu wakitengewa sh. milioni 72.2.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Chibe (CCM), Peter Kisandu, alisema makundi yote yamehamasika kukopa baada ya kuunda vikundi vitatu katika kata yake, ambavyo vilikopeshwa sh. milioni 16.

Scanned with CamScanner

# Samaki wanaoelea wazua taharuki ufukwe bahari ya Hindi Dar

HABARI UK. 3

Uhuru , Uk.1

Scanned with CamScanner